# UTANGULIZI

## KWA JINA LA BABA NA MWANA NA ROHO MTAKATIFU, AMIN.

KWA VILE ni kanuni ya Kanisa Anglikana ulimwenguni ambalo ni sehemu ya Kanisa Katholiko kwamba Dayosisi kadhaa ziungane pamoja na kuunda Jimbo;

NA KWA VILE Dayosisi za Zanzibar na Tanga, Dar es Salaam, Masasi, Morogoro, South-West Tanganyika, Western Tanganyika, Victoria Nyanza na Central Tanganyika zilikwisha kuungana na kufanya Kanisa Anglikana Tanzania;

ILIVYOKUWA KWAMBA tokea zama za Mitume kumekuwepo Daraja za Maaskofu, Makasisi, Mashemasi pamoja na Walei katika kuhudumia Kanisa la Kristo;

NA KWA KUWA kwa kufuatana na mafundisho ya Kikristo wanadamu wote wana thamani na ustahivu sawa mbele za Mungu;

NA INGAWA Kanisa linachukua hadhari katika kutimiza haja maalum za watu wa aina mbalimbali lililokabidhiwa;

HATA HIVYO Kanisa haliruhusu ubaguzi wowote usababishwao na tofauti za kitaifa juu ya watu wake wala katika utawala wake;

NA KWA KUWA imeonekana kuwa ni muhimu kuipitia na kuirekebisha Katiba hii, ili kukidhi haja za sasa na kutokana na kuongezeka kwa idadi za Dayosisi, na kupanuka kwa huduma za Kanisa;

KWA HIYO BASI, KATIBA HII imefanyiwa marekebisho ya kina na Sinodi ya Kanisa

Anglikana Tanzania iliyokutana Dodoma katika mwaka wa Bwana wetu Yesu Kristo wa 2004.

## SURA YA KWANZA

## JINA

### KIFUNGU CHA KWANZA

**Jina la Katiba**

1. Kutakuwepo na Kanisa Anglikana Tanzania lililoandikishwa kisheria Na. SO4057 litakaloendeshwa kwa mujibu wa Katiba hii.

2. Jina la Katiba hii ni "Katiba ya Kanisa Anglikana Tanzania, 1970".

### KIFUNGU CHA PILI

**Ufafanuzi**

Katika Katiba hii, ila iwapo maelezo yahitaji vinginevyo:

**"CMM"** ina maana ya "Chama cha Mariamu Mbarikiwa" ambacho ni chama cha watawa wanawake (Masista).

**"Daraja Takatifu"** ina maana ya mojawapo ya daraja ya Huduma ya Kuamriwa, yaani, Shemasi au Kasisi au Askofu.

**"Dayosisi"** ina maana eneo la Kanisa lililoidhinishwa na Katiba hii linaloongozwa na Askofu.

**"Halmashauri ya Kudumu"** ina maana ya Kamati ya Utendaji iliyoteuliwa na Sinodi ya Kanisa yenye mamlaka ya kuendesha kazi za Kanisa kati ya vikao kama ilivyoundwa chini ya Kifungu 24 cha Katiba hii.

**“Huduma Takatifu”** ina maana ya Huduma itolewayo na wale waliomo katika Daraja Takatifu.

**“Kamati ya Katiba”** ina maana ya Kamati ya Kanisa ya kushughulikia mambo ya Katiba hii na Katiba za Dayosisi na masuala yote ya kisheria iliyoundwa chini ya Kanuni 10 ya Katiba hii.

**“Kamati Maalum ya Muda”** ina maana ya Kamati iliyoundwa kwa muda ya kushughulikia uchaguzi wa Askofu wa Dayosisi chini ya Kifungu 12 cha Katiba hii.

**“Kanisa”** ina maana ya Kanisa Anglikana Tanzania.

**“Katibu Mkuu wa Kanisa”** ina maana ya Katibu aliyeteuliwa na Nyumba ya Maaskofu kwa mujibu wa Kanuni 6 ya Katiba hii.

**“Kitabu cha Sala”** ina maana ya Kitabu cha Sala cha Kanisa Anglikana Tanzania.

**“Mfuko wa Akiba wa Kanisa”** ina maana Mfuko ulioanzishwa chini ya Kanuni ya 11 (Provincial Provident Fund).

**“Mlei”** ina maana ya Mkristo ambaye hakuamriwa katika Daraja Takatifu.

**“Msajili wa Kanisa”** ina maana ya Mwanasheria ambaye ameteuliwa na Sinodi ya Kanisa kuwa mshauri wa Askofu Mkuu na wa Kanisa wa mambo yote yanayohusu sheria.

**“Mshiriki”** ina maana ya Mkristo anayepokea Ushirika Mtakatifu si chini ya mara sita kwa mwaka.

**“Mtaa”** ina maana eneo lenye mkusanyiko wa waumini walio chini ya uangalizi wa Kasisi mwenye idhini ya Askofu.

**"Sinodi ya Kanisa"** ina maana ya kikao kikuu kabisa katika utawala wa Kanisa kilichowekwa chini ya Kifungu 23 cha Katiba hii.

**"UMAKI"** ina maana ya "Ushirika wa Mama wa Kikristo".
"**TAYO**" ina maana Tanzania Anglican Youth Organization.

**"Tume ya Muda"** ina maana ya Tume itakayoundwa na Askofu Mkuu chini ya Kanuni 7 ya Katiba hii.

**"Vijana"** ina maana ya wavulana na wasichana wenye umri wa miaka kati ya 18 hadi 35.

**"Kamati ya Fedha"** ina maana Kamati ya Kanisa ya kushughulikia masuala yote ya fedha za Kanisa iliyoundwa chini ya Kanuni 5 ya Katiba hii.

**"Katholiko"** ina maana ya ushirika wa watu wote waaminio nyakati zote na mahali pote.

## SURA YA PILI

## ENEO LA KANISA

### KIFUNGU CHA TATU

**Eneo la Kanisa**

(1) Eneo la Kanisa litakuwa eneo lote la Dayosisi zifuatazo:-
- (a) Dayosisi ya Zanzibar - 1892
- (b) Dayosisi ya Masasi - 1926
- (c) Dayosisi ya Central Tanganyika - 1927
- (d) Dayosisi ya South West Tanganyika - 1952
- (e) Dayosisi ya Victoria Nyanza - 1963
- (f) Dayosisi ya Morogoro - 1965
- (g) Dayosisi ya Dar es Salaam - 1965
- (h) Dayosisi ya Western Tanganyika - 1966
- (i) Dayosisi ya Ruvuma - 1971

(j) Dayosisi ya Mount Kilimanjaro - 1982
(k) Dayosisi ya Kagera - 1985
(l) Dayosisi ya Mara - 1985
(m) Dayosisi ya Tabora - 1989
(n) Dayosisi ya Ruaha - 1990
(o) Dayosisi ya Mpwapwa - 1991
(p) Dayosisi ya Rift Valley - 1991
(q) Dayosisi ya Southern Highlands - 1999
(r) Dayosisi ya Tanga - 2000
(s) Dayosisi ya Kondoa - 2001

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, zinaweza kuanzishwa Dayosisi nyingine katika eneo la Kanisa kwa mujibu wa Katiba hii.

(3) Kanisa ni sehemu ya Kanisa Anglikana ulimwenguni kote katika ushirika wa Kanisa Moja, Takatifu, Katholiko na Apostoliko; likiwa na uhusiano wa kihistoria na Askofu Mkuu wa Canterbury.

(4) Kwa mujibu wa Katiba hii, Sinodi ya Kanisa inaweza kuingiza katika eneo la Kanisa Dayosisi nyingine ya Kanisa Anglikana katika sehemu zinazopakana na Tanzania.

(5) Kanisa linaweza kuungana na Jimbo au Majimbo mengine ya Kanisa Anglikana katika kuunda Jimbo au Majimbo mapya.

(6) Dayosisi itakuwa na haki ya kujitoa katika Kanisa na kujiunga kama Dayosisi katika Jimbo la Kanisa Anglikana jingine, baada ya Sinodi ya Dayosisi hiyo kupeleka ombi hilo kwenye Nyumba ya Maaskofu na baada ya Nyumba ya Maaskofu kulifikisha kwenye Sinodi ya Kanisa na kuidhinishwa.

# SURA YA TATU

# MAMBO YA IMANI

## KIFUNGU CHA NNE

**Misingi ya Elimu ya Dini**

(1) Kanisa linapokea misingi ifuatayo kuwa ndiyo yenye elimu yote iliyo lazima kwa wokovu:-

(a) Maandiko Matakatifu yaliyomo katika Agano la Kale na Agano Jipya kuwa ndiyo kanuni ya msingi wa Imani, yakiwa yametolewa kwa pumzi ya Mungu.

(b) Imani ya Mitume na Imani ya Nikea kuwa ni Mihutasari ya Imani.

(c) Mwongozo wa Ibada kama ulivyo katika Kitabu cha Sala cha Kanisa Anglikana Tanzania

(2) Kanisa linakataza haki yoyote ya kuhitilafiana na misingi ya Imani na Kanuni (Faith and Order) au Kanuni za Ibada kama zilivyopokelewa na kuhifadhiwa katika Kitabu cha Sala cha Jimbo na Kitabu cha Sala kwa Watu Wote cha Mwaka 1662 (**Book of Common Prayers 1662)**.

(3) Kanisa linaweza kufanya mabadiliko au nyongeza katika Kitabu cha Sala.

(4) Katika kutafsiri misingi na maandishi hayo yaliyokwisha kutajwa, na katika masuala yote ya Imani, Elimu ya Dini, Maadili, Marudi na Ibada, Kanisa halifungwi na uamuzi mwingine isipokuwa ule wa Sinodi ya Kanisa.

## SURA YA NNE

## IBADA

### KIFUNGU CHA TANO

**Liturgia**

(1) Dayosisi zote katika ibada zao zote zitatumia Kitabu cha Sala.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, ibada maalum ambazo hazimo katika Kitabu cha Sala zinaweza kufanyika kwa idhini ya Askofu wa Dayosisi.

## SURA YA TANO

## KUHUSU HUDUMA

### KIFUNGU CHA SITA

**Kuhusu Huduma**

(1) Kanisa litahudumiwa kama ielezwavyo katika Kifungu hiki:

(a) Kutakuwepo na Daraja Takatifu ambalo ni Shemasi, Kasisi na Askofu.

(b) Kutakuwepo na Huduma ya Walei ambao watatoa huduma kama itakavyoelezwa na Katiba za Dayosisi.

(2) Mtu yeyote asihesabiwe wala kufikiriwa kuwemo katika Daraja Takatifu isipokuwa ameitwa, amejaribiwa, amepimwa na kuamriwa kwa Huduma Takatifu kwa mujibu wa Ibada ya Kuamuru Wahudumu kama ilivyo katika Kitabu cha Sala.

(3) Wale wote walio kwenye Daraja Takatifu katika Dayosisi yoyote ya Kanisa Anglikana ambayo imejiunga na Kanisa kwa mujibu wa Kifungu cha 3(4) cha Katiba hii, watatambuliwa moja kwa moja chini ya kifungu kidogo cha (2) cha Kifungu hiki.

(4) Kasisi, Shemasi na Mlei aliyeruhusiwa kutoa huduma katika Dayosisi yoyote ya Kanisa hana budi kuitii ilivyo kanuni Askofu wa Dayosisi hiyo katika mambo yote ya halali na haki.

(5) Askofu wa Dayosisi, Kasisi, Shemasi na Mlei katika Dayosisi yoyote hana budi kuitii ilivyo kanuni Katiba ya Dayosisi inayohusika.

(6) Kila Askofu wa Dayosisi yoyote hana budi kuitii ilivyo kanuni Askofu Mkuu na Katiba hii.

(7) Mlei, Shemasi na Kasisi atalazimika kustaafu afikiapo umri wa miaka sitini na tano (65).

Isipokuwa Askofu wa Dayosisi anaweza kumwomba Shemasi au Kasisi aliyestaafu kwa mkataba wa vipindi visivyozidi jumla ya miaka mitano.

## SURA YA SITA

## ASKOFU MKUU

### KIFUNGU CHA SABA

**Askofu Mkuu na Uchaguzi**

(1) Kutakuwa na Askofu Mkuu atakayetimiza haki na wajibu wa kama inavyoagizwa na Katiba hii.

(2) (a) Askofu Mkuu atachaguliwa na Sinodi Maalum ya Kanisa ya Uchaguzi kutokana na Maaskofu wa Dayosisi au Maaskofu wa Dayosisi Wateule wenye umri usiozidi miaka sitini (60).

(b) Utaratibu wa uchaguzi wake utakuwa kama unavyoagizwa katika Kanuni ya 1 ya Katiba hii.

**KIFUNGU CHA NANE**

**Muda na Madaraka**

(1) Askofu Mkuu atashika madaraka yake kwa kipindi cha miaka mitano lakini anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

(2) Endapo Askofu Mkuu hawezi kutimiza wajibu wake kutokana na ugonjwa wa mwili au akili, Nyumba ya Maaskofu, kwa kauli ya wingi wa kura, itakuwa na mamlaka ya kumwachisha madaraka Askofu Mkuu, na kuiarifu Sinodi, na utaratibu wa uchaguzi utafuata.

Isipokuwa kwamba hatua hiyo haitachukuliwa mpaka ushauri huo umepatikana kutoka kwa jopo la madaktari wasiopungua watatu.

(3) Askofu Mkuu anaweza kuachishwa huduma yake wakati wowote ikiwa baada ya uchunguzi wa kutosha na Nyumba ya Maaskofu, wakifuata lalamiko lililoletwa kama ilivyo kanuni, Askofu Mkuu akaonekana kuwa anayo hatia kuhusu tabia isiyofaa kwa cheo na huduma ya Askofu Mkuu au ikiwa anaendelea kutojali wajibu wake.

(4) Askofu Mkuu atalazimika kuacha wadhifa wake baada ya vipindi viwili vya miaka mitano kila kimoja, na kwa vyovyote vile

hataweza kuwa Askofu Mkuu ikiwa ametimiza umri wa miaka sitini na tano (65).

(5) Ikiwa Askofu Mkuu ataacha kuwa Askofu wa Dayosisi katika Kanisa basi ataacha kuwa Askofu Mkuu.

(6) Kama Askofu Mkuu ataacha kuwa Askofu Mkuu lakini anaendelea kuwa Askofu wa Dayosisi, basi atatumia cheo cha Askofu wa Dayosisi na wala sio cheo cha Askofu Mkuu.

## KIFUNGU CHA TISA

**Madaraka ya Askofu Mkuu**

Askofu Mkuu, zaidi ya madaraka aliyo nayo kama Askofu wa Dayosisi, atakuwa na madaraka yafuatayo:-

(a) Uongozi na uangalizi wa Kanisa zima na Maaskofu wake kwa kufuata Katiba hii.

(b) Kumshauri Askofu wa Dayosisi kustaafu kwa mujibu wa Kifungu cha 18 (1)(d) cha Katiba hii na kama Askofu wa Dayosisi anayehusika akikataa kustaafu, kumuamuru astaafu.

(c) Kuitisha na kuwa Mwenyekiti wa Nyumba ya Maaskofu, Sinodi ya Kanisa na Halmashauri ya Kudumu.

(d) Kuongoza Dayosisi yoyote isiyokuwa na Askofu mpaka hapo Askofu wa Dayosisi atakapochaguliwa.

(e) Kuwa Mwenyekiti wakati wa kusikiliza rufani zozote kutoka uamuzi wa Dayosisi na wakati wowote Nyumba ya Maaskofu itakapokutana kama Baraza la Hukumu la Kanisa.

(f) Kutembelea rasmi Dayosisi yoyote ya Kanisa bila pingamizi yoyote.

(g) Kuliwakilisha Kanisa katika mikutano na Makanisa mengine ndani na nje ya nchi na serikali.

(h) Kusimamia taratibu za kugawa Dayosisi na kuweka wakfu Maaskofu

(i) Kuthibitisha uchaguzi wa Maaskofu na kupanga kuwaweka wakfu na kutawazwa kwao.

(j) Kutimiza wajibu mwingine wowote atakaokabidhiwa na Kanisa.

**KIFUNGU CHA KUMI**

**Kumtawaza Askofu Mkuu**

(1) Askofu Mkuu Mteule atatawazwa katika kipindi kisichozidi miezi mitatu tokea alipochaguliwa.

(2) Sherehe za kutawaza zitafanyika mahali yalipo Makao Makuu ya Kanisa kwa kushirikiana na Askofu wa Dayosisi/eneo husika na kuongozwa na Askofu Mkuu mstaafu au, kama hayupo, Askofu wa Dayosisi aliyewekwa wakfu awali ya wote.

(3) Idadi ya chini ya Maaskofu wa Dayosisi watakaoshiriki katika kumtawaza Askofu Mkuu ni watatu.

**KIFUNGU CHA KUMI NA MOJA**

**Makamu wa Askofu Mkuu (Dean)**

(1) Makamu wa Askofu Mkuu atateuliwa na Askofu Mkuu kwa kushauriana na Nyumba ya Maaskofu.

(2) Endapo Makamu wa Askofu Mkuu amefariki, au hawezi kwa sababu yoyote ile, Askofu aliyewekwa wakfu awali ya wote waliopo atakuwa badala yake mpaka uchaguzi mwingine utakapofanyika.

(3) Wakati wowote ambapo Kanisa litakuwa halina Askofu Mkuu au Askofu Mkuu hawezi, au hayupo katika mipaka ya eneo la Kanisa kwa muda unaozidi siku thelathini, Makamu wa Askofu Mkuu atachukua madaraka ya Askofu Mkuu.

(4) Makamu wa Askofu Mkuu atafanya shughuli nyingine atakazopangiwa na Askofu Mkuu

## SURA YA SABA

## MAASKOFU WA DAYOSISI

### KIFUNGU CHA KUMI NA MBILI

**Utaratibu wa kupendekeza majina ya wanaofikiriwa kwa nafasi ya Askofu ngazi ya Dayosisi**

(1) Kutakuwa na Askofu wa Dayosisi atakayetimiza haki na wajibu kama inavyoagizwa na Katiba hii pamoja na Katiba ya Dayosisi husika.

(2) Wakati wa uchaguzi wa Askofu wa Dayosisi yoyote, Halmashauri ya Kudumu ya Dayosisi itaunda Kamati Maalum ya Muda itakayokuwa na wajumbe kumi na moja kama ifuatayo;-

(a) Mwenyekiti - atakayeteuliwa na Halmashauri ya Kudumu;

(b) Wahudumu wanne – kati yao Makanoni wawili walio kazini;

(c) Walei sita – kati yao wanaume wawili, wanawake wawili na vijana wawili (mvulana mmoja na msichana mmoja wenye umri wa miaka kati ya 18 hadi 35).

(3) Kila Halmashauri ya Mtaa itapendekeza kwa Halmashauri ya Kudumu ya Dayosisi jina moja la Kasisi kutoka ndani au nje ya Dayosisi au nje ya Kanisa, mwenye sifa zilizotajwa katika Kanuni ya 2. Shughuli ya mapendekezo itasimamiwa na Katibu wa Mtaa.

(4) Kamati Maalum ya Muda ikiisha kupokea mapendekezo kutoka Halmashauri za Mitaa, yatakayowasilishwa kwake na Halmashauri ya Kudumu ya Dayosisi litachambua taarifa za waliopendekezwa kufuatana na vigezo vilivyowekwa na itapeleka mapendekezo yake kwa Halmashauri ya Kudumu ya Dayosisi ikiainisha wale waliostahili kufikiriwa na wale inayoona hawastahili na kutoa sababu zake.

(5) Halmashauri ya Kudumu ya Dayosisi baada ya kupokea taarifa ya mapendekezo ya Kamati Maalum ya Muda itachuja majina na kupendekeza majina yasiyopungua mawili na yasiyozidi matano kwa Nyumba ya Maaskofu ikiambatisha taarifa kamili zinazowahusu walioteuliwa, nyaraka na taarifa zote tangu ngazi ya Mitaa hadi Halmashauri ya Kudumu, na kutoa sababu ya kutopendekezwa majina yaliyoachwa.

## KIFUNGU CHA KUMI NA TATU

**Utaratibu wa kupendekeza majina ya wanaofikiriwa kwa nafasi ya Askofu ngazi ya Jimbo**

(1) Katibu Mkuu atawapelekea waliopendekezwa na Halmashauri ya Kudumu ya Dayosisi fomu ya kukubali au kukataa kufikiriwa kwa nafasi ya Askofu ngazi ya Jimbo.

(2) Katibu Mkuu atawasilisha kwenye Nyumba ya Maaskofu majina ya wale waliopendekezwa na waliorejesha fomu wakikubali kushiriki katika uchaguzi.

(3) Nyumba ya Maaskofu itayajadili majina yaliyowasilishwa kwao na inaweza kujadili majina yaliyopendekezwa na Mitaa na ambayo yalichujwa.

(4) Nyumba ya Maaskofu itarejesha kwenye Halmashauri ya Kudumu ya Dayosisi majina yasiyopungua mawili na yasiyozidi matatu kutokana na mapendekezo ya Halmashauri ya Kudumu pamoja na yale yaliyotoka kwenye Mitaa. Uamuzi wa Nyumba ya Maaskofu utakuwa wa mwisho.

## KIFUNGU CHA KUMI NA NNE

**Utaratibu wa kumchagua Askofu wa Dayosisi**

(1) Halmashauri ya Kudumu itaitangazia Mitaa majina yaliyorudi kutoka Nyumba ya Maaskofu, na kuyawasilisha kwenye Sinodi Maalum ya Dayosisi.

(2) Sinodi Maalum ya Dayosisi itafanya uchaguzi chini ya uenyekiti wa Askofu Mkuu, au Askofu wa Dayosisi atakayemteua.

(3) Wakati wa uchaguzi watakuwepo waangalizi wanne: wawili watakaochaguliwa na Sinodi Maalum ya Uchaguzi siku hiyo hiyo ya uchaguzi na wawili watakaoteuliwa na Askofu Mkuu.

Isipokuwa kwamba kila upande awepo mhudumu mmoja na mlei mmoja.

(4) Upigaji kura utakuwa wa kupunguza majina (elimination) kwa kura za siri na matokeo yatatangazwa kila hatua ya uchaguzi.

(5) Endapo kura ya mwisho itakuwa sare mara tatu, uchaguzi utaahirishwa na kurudiwa siku inayofuata.

(6) Askofu Mkuu au Askofu aliyeteuliwa naye kuwa msimamizi wa uchaguzi atamtangaza kuwa Askofu Mteule wa Dayosisi ambaye atapata kura zaidi ya nusu ya kura zote zilizopigwa ambazo hazikuharibika katika kura ya mwisho.

(7) Askofu Mkuu atatoa hati ya kuchaguliwa kuwa Askofu Mteule wa Dayosisi aliyetangazwa katika Kifungu cha 14(6).

(8) Matokeo ya uchaguzi huo ni ya mwisho, hayatapingwa popote na taratibu za kumweka wakfu na kumsimika Askofu Mteule zitafuata.

(9) Katika utaratibu wote wa uchaguzi uliotajwa katika kifungu hiki, Askofu Mkuu anaweza kumtuma Msajili au Katibu Mkuu au mtu mwingine yeyote na wakati wowote atakaoona unafaa, kuwa mshauri wa Halmashauri ya Kudumu au Kamati Maalum ya Muda.

**KIFUNGU CHA KUMI NA TANO**

**Uteuzi wa Askofu Msaidizi**

(1) Kutakuwepo na Askofu Msaidizi wa Dayosisi, kama itaonekana haja ya kuwa naye, kutokana na;

(a) Maoni ya Askofu wa Dayosisi mwenyewe kupeleka shauri hilo mbele ya Halmashauri ya Kudumu ya Dayosisi; au

(b) Ushauri wa Halmashauri ya Kudumu ya Dayosisi kwa Askofu wa Dayosisi.

(2) Askofu wa Dayosisi, baada ya ushauri wa Halmashauri ya Dayosisi au baada ya maoni yake kupata kibali cha Halmashauri ya Dayosisi, atawasilisha jina la mteule huyo kwa Askofu Mkuu ambaye atawasilisha jina hilo

Nyumba ya Maaskofu ambao watatoa ushauri wao.

(3) Kama Nyumba ya Maaskofu itamwidhinisha Askofu Msaidizi, Askofu wa Dayosisi atamteua rasmi kuwa Askofu Msaidizi.

(4) Askofu Msaidizi atafanya kazi zote atakazopangiwa na Askofu wa Dayosisi.

(5) Askofu Msaidizi ataacha kuwa Askofu Msaidizi endapo;

(i) Askofu wa Dayosisi aliyemteua atakoma kuwa Askofu wa Dayosisi.

(ii) Askofu Msaidizi mwenyewe atakapojiuzulu kwa sababu yoyote ile.

(iii) Askofu wa Dayosisi atakapomtaka Askofu Msaidizi ajiuzulu.

(6) Panaweza kuwa na aina nyingine ya maaskofu wasiokuwa wa dayosisi ambao watateuliwa au kuchaguliwa kwa kufuata utaratibu wa uchaguzi wa Askofu wa Dayosisi au Askofu Msaidizi kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

**KIFUNGU CHA KUMI NA SITA**

**Kuwekwa wakfu Askofu**

(a) Punde tu baada ya uchaguzi wa Askofu wa Dayosisi, hatua za kumweka wakfu na kumtawaza zitafuata.

(b) Kila Askofu wa Dayosisi kabla ya kushika wadhifa wake atakula kiapo cha utii kwa Askofu Mkuu, Katiba hii na Katiba ya Dayosisi kama vilivyoainishwa katika Katiba hii.

(c) Punde tu baada ya uteuzi wa Askofu Msaidizi wa Dayosisi, hatua za kumweka wakfu zitafuata.

(d) Kila Askofu Msaidizi wa Dayosisi, kabla ya kushika wadhifa wake atakula kiapo cha utii kwa Askofu Mkuu, Katiba hii, Askofu wa Dayosisi na Katiba ya Dayosisi kama vilivyoainishwa katika Katiba hii.

**KIFUNGU CHA KUMI NA SABA**

**Viapo vya Askofu**

**(1) KIAPO CHA UTII KWA ASKOFU MKUU**

Katika Jina la Mungu. Amin. Mimi …………….niliyechaguliwa kuwa Askofu wa Kanisa na Dayosisi ya ……………nakubali na kuahidi kumheshimu na kumtii, kama inipasavyo, Askofu Mkuu wa Kanisa Anglikana Tanzania…………...na watakaofuata baada yake; kwa hiyo Ee Mwenyezi Mungu nisaidie. Amin.

**(2) KIAPO CHA UTII KWA KATIBA YA JIMBO**

Mimi…………..niliyechaguliwa kuwa Askofu wa Dayosisi ya ………………..

Ninaahidi kwamba nitaifundisha na kuitii Imani ya Bwana wetu YESU KRISTO na Elimu ya Dini na Taratibu na Maadili na Marudi kama alivyoamuru kwa Kanisa lake, na kama ilivyokubaliwa na kuelekezwa na Kanisa Anglikana Tanzania katika Katiba ya Kanisa hili.

NINAAHIDI pia kwamba ninakubali kufungwa na sheria na kanuni zote zilizowekwa na zitakazowekwa tangu sasa na Sinodi ya Kanisa Anglikana Tanzania.

NINAAHIDI pia kwamba nitakubali kujiuzulu au kujitoa kwa hukumu yoyote itakayoniachisha madaraka na mapato yanayohusika na Dayosisi hii nitakayohukumiwa wakati wowote baada ya uchunguzi wa kutosha wa Baraza lenye kibali cha Sinodi ya Kanisa.

Kiapo hiki kimetolewa nami na kutiwa sahihi yangu, leo tarehe…..ya mwezi wa……katika mwaka wa Bwana wetu Yesu Kristo wa …………………….

## (3) KIAPO CHA UTII KWA KATIBA YA DAYOSISI

Mimi……………..niliyechaguliwa kuwa Askofu wa Dayosisi ya …………………..

NINAAHIDI kwamba nitaiangalia misingi, sheria na masharti ya Dayosisi hii kama yatakavyoundwa mara kwa mara na Sinodi ya Dayosisi hii

NINAAHIDI pia kwamba nitaitisha vikao vya Sinodi ya Dayosisi kwa nyakati za kawaida kadri itakavyotakiwa mara kwa mara kufuata maazimio ya Sinodi.

NINAAHIDI pia kwamba nitakubali kustaafu kazi nifikiapo umri wa miaka 65.

NINAAHIDI pia kwamba nitajiuzulu wakati wowote kama ikiazimiwa na Askofu Mkuu wa Kanisa Anglikana Tanzania kwa mujibu wa Katiba ya Kanisa na ya Dayosisi hii. Mwenyezi Mungu anisaidie.

Kiapo hiki kimetolewa nami na kutiwa sahihi yangu leo, tarehe ……mwezi wa ……..katika mwaka wa Bwana wetu Yesu Kristo wa…………..

**Askofu Msaidizi pia atakula kiapo cha utii kwa Askofu wa Dayosisi na Katiba ya Dayosisi**

### (1) KIAPO KWA ASKOFU WA DAYOSISI

Katika Jina la Mungu. Amin. Mimi ……………niliyeteuliwa kuwa Askofu Msaidizi wa Kanisa na Dayosisi ya ……………nakubali na kuahidi kumheshimu na kumtii, kama inipasavyo, Askofu wa Dayosisi ……..na watakaofuata baada yake; kwa hiyo Mungu anisaidie kwa Yesu Kristo. Amin.

### (2) KIAPO KWA KATIBA YA DAYOSISI

Mimi……………niliyeteuliwa kuwa Askofu Msaidizi wa Dayosisi ya …………………..
NINAAHIDI kwamba nitaiangalia misingi, sheria na masharti ya Dayosisi hii kama yatakavyoundwa mara kwa mara na Sinodi ya Dayosisi hii

NINAAHIDI pia kwamba nitakubali kustaafu kazi nifikiapo umri wa miaka 65.

NINAAHIDI pia kwamba nitajiuzulu wakati wowote kama ikiazimiwa na Askofu wa Dayosisi kwa mujibu wa Katiba ya Kanisa na ya Dayosisi hii. Mwenyezi Mungu anisaidie.

Kiapo hiki kimetolewa nami na kutiwa sahihi yangu leo, tarehe ……mwezi wa ……..katika mwaka wa Bwana wetu Yesu Kristo wa…………..

### KIFUNGU CHA KUMI NA NANE

**Kuacha Madaraka ya Askofu**

(1) Askofu wa Dayosisi ataacha madaraka ya Askofu wa Dayosisi litokeapo lolote kati ya yafuatayo:-

   (a) Akijiuzulu kwa hiari yake mwenyewe wakati wowote.

   (b) Akitimiza umri wa miaka sitini na tano (65).

(c) Endapo Askofu wa Dayosisi hawezi kutimiza wajibu wake kutokana na ugonjwa wa mwili au akili, Nyumba ya Maaskofu, kwa kauli ya wingi wa kura, itakuwa na mamlaka ya kumwachisha madaraka Askofu wa Dayosisi, na utaratibu wa uchaguzi utafuata.

Isipokuwa kwamba hatua hiyo haitachukuliwa mpaka ushauri huo umepatikana kutoka kwa jopo la madaktari wasiopungua watatu.

(d) Amethibitishwa na Nyumba ya Maaskofu kuwa anayo imani na tabia isiyofaa kwa cheo na huduma ya Askofu wa Dayosisi au ikiwa anaendelea kutojali wajibu wake na kama Askofu Mkuu amemshauri kustaafu.

(e) Ameamriwa kujiuzulu na Askofu Mkuu kwa mujibu wa Kifungu 9(b) cha Katiba hii.

(2) Askofu Msaidizi ataacha madaraka ya Askofu Msaidizi litokeapo lolote la yafuatayo:-

(a) Yaliyotajwa kwenye Kifungu Kidogo (1) cha Kifungu hiki.

(b) Kama ametawazwa Askofu wa Dayosisi mpya na ambaye hakuidhinisha Askofu Msaidizi aliyekuwepo kuendelea na wadhifa huo.

## SURA YA NANE

## DAYOSISI

### KIFUNGU CHA KUMI NA TISA

**Katiba za Dayosisi za Kanisa**

(a) Kila Dayosisi itakuwa na Katiba yake ambayo itatambua kuwepo kwa Nyumba Tatu, yaani Askofu wa Dayosisi, Nyumba ya Wahudumu na Nyumba ya Walei.

(b) Kila Katiba ya Dayosisi itabidi iwe imekubaliwa na Sinodi ya Dayosisi na kuthibitishwa na Sinodi ya Kanisa.

(c) Hakuna rekebisho lolote litakaloweza kufanywa katika Katiba ya Dayosisi isipokuwa pale rekebisho hilo litakapokuwa limeidhinishwa na Sinodi ya Kanisa au Halmashauri ya Kudumu ya Kanisa kwa niaba ya Sinodi ya Kanisa.

(d) Iwapo kifungu, au sehemu yoyote katika Katiba ya Dayosisi inapingana na Katiba hii katika suala lolote, basi Katiba ya Kanisa ndiyo itakayotumika katika mambo yote ya jumla.

### KIFUNGU CHA ISHIRINI

**Uhusiano wa Dayosisi na Dayosisi**

(a) Kila Askofu wa Dayosisi ataheshimu madaraka na mipaka ya Dayosisi ya Askofu wa Dayosisi nyingine.

(b) Mipaka ya Dayosisi mpya ifuate kwa kadri inavyowezekana au kuonekana inafaa mipaka ya kiutawala ya wilaya za Serikali.

(c) Shemasi au Kasisi wa Dayosisi moja anaweza kuhamia kwenye Dayosisi nyingine baada ya mashauriano kufanyika kati ya Askofu wa Dayosisi yake na Askofu wa Dayosisi ile anayokwenda kutoa huduma.

**KIFUNGU CHA ISHIRINI NA MOJA**

**Kugawa Dayosisi**

Dayosisi inaweza kugawanywa na kufanywa Dayosisi mbili au zaidi au inaweza kumegwa na sehemu yake kuungwa na Dayosisi nyingine au sehemu ya Dayosisi nyingine ili kuunda Dayosisi mpya kama inavyoelezwa katika Kanuni ya 7 ya Katiba hii.

**KIFUNGU CHA ISHIRINI NA MBILI**

**Kanisa Kuu na Baraza la Ushauri**

1. Kila Dayosisi itakuwa na Kanisa Kuu (Cathedral) ambalo litaongozwa na Dean ambaye anaweza kuwa Askofu wa Dayosisi au Kasisi atakayeteuliwa na Askofu.

2. Kutakuwepo na Baraza la Kanisa Kuu (Cathedral Chapter) katika kila Dayosisi kulingana na Katiba ya Dayosisi.

## SURA YA TISA

## VIKAO VYA KANISA

**KIFUNGU CHA ISHIRINI NA TATU**

**Sinodi ya Kanisa**

Kutakuwa na Sinodi ya Kanisa ambayo itakuwa na nyumba tatu, Yaani Nyumba ya Maaskofu, Nyumba ya Wahudumu na Nyumba ya Walei. Wajumbe wa Sinodi watakuwa kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 3.

## KIFUNGU CHA ISHIRINI NA NNE

**Vikao vya Sinodi**

(1) Sinodi ya Kanisa itakuwa na Kikao cha Kawaida (Ordinary Session) mara moja katika miaka mitatu wakati na mahali patakapochaguliwa na Askofu Mkuu.

(2) Sinodi ya Kanisa inaweza kuwa na Kikao Maalum (Extra Ordinary Session) kwa kuitishwa na Askofu Mkuu kutokana na lolote la yafuatayo:

(a) uamuzi wake mwenyewe Askofu Mkuu;

(b) pendekezo la Halmashauri ya Kudumu ya Sinodi;

(c) pendekezo la theluthi mbili ya Dayosisi zote za Kanisa kwa kupitia Halmashauri za Kudumu za Dayosisi hizo.

(3) Askofu Mkuu atakuwa Mwenyekiti wa Kikao cha Sinodi ya Kanisa. Isipokuwa kama hawezi au hayupo:

(a) Makamu wa Askofu Mkuu (Dean); au

(b) Askofu wa Dayosisi aliyewekwa wakfu awali ya wote (the most Senior Bishop).

(4) (a) Idadi ya chini ya wajumbe wa Sinodi ya Kanisa ili kikao kifanyike ni:

(i) nusu ya wajumbe wote; na

(ii) kila Nyumba isiwe chini ya theluthi moja ya wajumbe wake.

(b) Kama idadi iliyotajwa katika ibara (a) haikutimia, Mwenyekiti ataahirisha kikao kwa muda atakaoona unafaa.

(5) Utaratibu wa agenda za Sinodi za Kanisa utakuwa kama ielezwavyo katika Kanuni ya 9.

**KIFUNGU CHA ISHIRINI NA TANO**

**Madaraka ya Sinodi**

(1) Sinodi ya Kanisa itakuwa na madaraka yafuatayo:-

(a) Kutoa maamuzi ya mwisho kuhusu mambo yote ya mwenendo wa kiroho katika Kanisa.

(b) Kutekeleza mambo hayusuyo Kanisa zima na yale yanayohusu uhusiano wa Dayosisi moja na nyingine na uhusiano wa Kanisa na Majimbo mengine ya Kanisa Anglikana.

(c) Kupokea na kuidhinisha maombi kutoka Sinodi ya Dayosisi yoyote ya kuigawa au kuimega Dayosisi.

(d) Kuwachagua Maafisa wa Kanisa chini ya Kifungu cha ishirini na sita (isipokuwa Askofu Mkuu na Katibu Mkuu) na wajumbe wa Halmashauri ya Kudumu chini ya Kifungu ishirini na saba 2(c) Kupokea na kuidhinisha maombi kutoka Sinodi za Dayosisi yoyote ya kuigawa au kuimega Dayosisi.

(e) Kuunda Kamati na Bodi za Kanisa kama zitakavyohitajiwa.

(f) Kuidhinisha mabadiliko ya Katiba za Dayosisi.

(g) Kupitisha marekebisho ya Katiba hii.

(h) Kusikiliza rufani kutoka Baraza la Dayosisi hadi kwenye Baraza la Kanisa kwa mambo yale tu yanayotajwa katika Katiba za Dayosisi.

(i) Kusimamia shughuli za maendeleo, biashara na vitega uchumi.

(j) Kupokea na kupitisha hesabu za fedha na mali za Kanisa zilizokaguliwa.

(k) Kuteua Wakaguzi wa Nje wa fedha na mali za Kanisa.

(2) Maamuzi ya Sinodi ya Kanisa yatatolewa kama Amri za Sinodi na zitapewa namba katika mtiririko. Maamuzi lazima yapitishwe na kukubaliwa na Nyumba zote tatu.

Isipokuwa maamuzi ya Sinodi ya Kanisa kuhusu Kifungu 4 cha Katiba hii yasipitishwe mpaka yamekubaliwa na Nyumba ya Maaskofu na kuidhinishwa na Askofu Mkuu kwa maandishi.

## KIFUNGU CHA ISHIRINI NA SITA

**Sinodi Maalum ya Kanisa ya Uchaguzi**

(1) Kutakuwepo na Sinodi Maalum ya Kanisa ya uchaguzi ambayo kazi yake itakuwa kumchagua Askofu Mkuu na Makamu wa Askofu Mkuu tu.

(2) Wajumbe wa Sinodi Maalum ya Kanisa ya uchaguzi ni wale wale ambao ni wajumbe wa Sinodi ya Kanisa.

## KIFUNGU CHA ISHIRINI NA SABA

**Maafisa wa Kanisa**

(1) Kutakuwa na Maafisa wa Kanisa ambao ni:-
(a) Askofu Mkuu;
(b) Makamu wa Askofu Mkuu (Dean);
(c) Mhazini wa Kanisa;
(d) Msajili wa Kanisa; na
(e) Katibu Mkuu wa Kanisa.

(2) Maafisa wa Kanisa watakuwa na wajibu ufuatao:

(a) Kuajiri, kupandisha daraja kuachisha au kufukuza kazi watumishi wa Sekretariati na Kanisa.

(b) Kuangalia na kusimamia utendaji kazi wa watumishi wa Secretariati ya Kanisa.

(c) Kukusanya na kuyachambua mapendekezo ya agenda za Sinodi ya Kanisa na Halmashauri za Kudumu.na kuwasilisha kwenye Nyumba ya Maaskofu

(d) Kusimamia uendeshaji wa siku kwa siku wa Kanisa

(e) Kupokea mapendekezo ya Kanuni za Utumishi na kutoka Kamati ya Fedha na kuyapitisha

(f) Kupokea taarifa za mahesabu yaliyokaguliwa na kazi za maendeleo za Idara na Taasisi za Kanisa, na kutoa maamuzi kama watakavyoona inafaa.

(g) Kutekeleza madaraka mengine kama itakavyoagizwa na Kanuni za Sinodi ya Kanisa na Halmashauri ya Kudumu.

## KIFUNGU CHA ISHIRINI NA NANE

**Halmashauri ya Kudumu**

Kutakuwepo na Halmashauri ya Kudumu ya Kanisa.

(1) Wajumbe wa Halmashauri ya Kudumu watakuwa wafuatao:-

- (a) Wajumbe kwa sababu ya vyeo vyao:-
  - (i) Maafisa;
  - (ii) Maaskofu wote wa Dayosisi;
  - (iii) Mwenyekiti wa Nyumba ya Wahudumu ya Sinodi;
  - (iv) Mwenyekiti wa Nyumba ya Walei ya Sinodi;
  - (v) Mwenyekiti wa UMAKI;
  - (vi) Mwenyekiti wa TAYO; na
  - (vii) Mama Mkuu wa CMM .

- (b) Wajumbe wa kuchaguliwa na Sinodi ya Kanisa:
  - (i) Wajumbe watatu wa Nyumba ya Wahudumu;
  - (ii) Wajumbe watatu wa Nyumba ya Walei;
  - (iii) Wajumbe wawili TAYO; na
  - (iv) Wajumbe wawili UMAKI.

(2) (a) Halmashauri ya Kudumu itakutana mara moja kila mwaka isipokuwa mwaka wa Kikao cha Sinodi. Askofu Mkuu anaweza kuitisha kikao cha dharura cha Halmashauri ya Kudumu.

(b) Akidi (quorum) ya mkutano wa Halmashauri ya Kudumu ni nusu ya wajumbe wote ambao kati yao awepo mjumbe mmoja kutoka kila Nyumba ya Sinodi.

(3) Kazi za Halmashauri ya Kudumu zitakuwa:

(i) Kutekeleza shughuli za Sinodi ya Kanisa kati ya vikao vya Sinodi.
(ii) Kutekeleza shughuli nyingine zozote zilizoelezwa katika Kanuni za Katiba hii.

## KIFUNGU CHA ISHIRINI NA TISA

**Nyumba ya Maaskofu**

(1) Kutakuwepo Nyumba ya Maaskofu ambayo itakuwa na Maaskofu wa Dayosisi zote za Kanisa.

(2) Majukumu ya Nyumba ya Maaskofu yatakuwa yafuatayo:-

(a) Kujadili, kuamua na kupeleka kwenye Sinodi ya Kanisa jambo lolote linalohusu Imani na Kanuni (Faith and Order).

(b) Kutaka ushauri toka Halmashauri ya Mashauriano ya Kanisa ya Mkutano wa Lambeth (Anglican Consultative Council of the Lambeth Conference) au tume yake yoyote ikiwa Nyumba ya Maaskofu itakuwa na shaka, au haikubaliani katika jambo linalohusu Imani na Kanuni (Faith and Order) na kama walau Maaskofu wawili wataomba iwe hivyo.

(c) Kuteua Katibu Mkuu wa Kanisa.

(d) Kuwa Baraza la Rufaa la Kanisa (Provincial Tribunal) kwa mambo yote yanayohusu Kanisa, kufanya tafsiri ya Katiba hii.

Askofu wa Dayosisi anayehusika na rufani iliyo mbele ya Baraza, atahudhuria vikao kama Baraza litaamua kumwita, lakini hatashiriki katika kutoa hukumu.

(e) Kuandaa agenda ya mkutano wa Sinodi ya Kanisa na Halmashauri ya Kudumu.

(3) Uamuzi wa Nyumba ya Maaskofu utakuwa kwa wingi wa kura, za wazi au za siri, za Maaskofu waliohudhuria.

## KIFUNGU CHA THELATHINI

**Nyumba ya Wahudumu**

(1) Nyumba ya Wahudumu itakuwa na wajumbe wawili walio Wahudumu kutoka kila Dayosisi.

(2) Maaskofu Wasaidizi wanaweza kuchaguliwa kuwa wajumbe wa Nyumba ya Wahudumu.

(3) Nyumba ya Wahudumu itakapokutana watachagua miongoni mwao Mwenyekiti na Katibu wao.

(4) Akidi (quorum) kwa ajili ya kikao cha Nyumba ya Wahudumu itakuwa nusu ya wajumbe wote.

## KIFUNGU CHA THELATHINI NA MOJA

**Nyumba ya Walei**

(1) Nyumba ya Walei itakuwa na wajumbe Walei wawili walio washiriki wa Kanisa wenye umri usiopungua miaka kumi na minane waliochaguliwa kutoka kila Dayosisi ya Kanisa.

(2) Nyumba ya Walei itakapokutana watachagua miongoni mwao Mwenyekiti na Katibu wao.

(3) Akidi (quorum) kwa kikao cha Nyumba ya Walei itakuwa nusu ya wajumbe wote.

## SURA YA KUMI

## WADHAMINI WA KANISA

### KIFUNGU CHA THELATHINI NA MBILI

**Wadhamini wa Kanisa**

(1) Kutakuwa na Wadhamini wa Kanisa ambao ni Nyumba ya Maaskofu.

(2) Mali yote, ikiwa thabiti au isiyo thabiti, ya Kanisa na itakayopokelewa na Kanisa itakabidhiwa kwa Wadhamini wa Kanisa.

(3) Uuzaji, ununuzi au ubadilishanaji wa mali ya Kanisa utahitaji idhini ya Wadhamini wa Kanisa wakiwakilishwa na Maaskofu wa Dayosisi wawili, akiwamo Askofu wa Dayosisi inayohusika.

(4) Katika utekelezaji wa ibara (3), Wadhamini wa Kanisa watashauriana na Msajili na Katibu Mkuu.

## SURA YA KUMI NA MOJA

## UTUNGAJI WA KANUNI ZA KANISA

### KIFUNGU CHA THELATHINI NA TATU

**Utungaji wa Kanuni za Kanisa**

(1) Zitatungwa Kanuni za Kanisa ambazo zitakuwa sehemu ya Katiba hii.

(2) Kanuni za Kanisa zitaweka utaratibu wa utekelezaji wa vifungu vya Katiba hii.

(3) Kanuni za Kanisa zitatungwa, zitarekebishwa, au kufutwa na Halmashauri ya Kudumu kwa kura ya theluthi mbili ya wajumbe wote.

(4) Halmashauri ya Kanisa itatoa taarifa kwa Sinodi ya Kanisa kuhusu hatua yoyote itakayochukua chini ya ibara (3).

## SURA YA KUMI NA MBILI

## MAREKEBISHO YA KATIBA

### KIFUNGU CHA THELATHINI NA NNE

**Marekebisho ya Katiba**

(1) Katiba hii inaweza kufanyiwa marekebisho kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na kifungu hiki.

(2) Kamati ya Katiba iliyoundwa chini ya Kanuni ya 10 ya Katiba hii, itatoa mapendekezo ya kurekebisha Katiba na, baada ya kupata idhini ya Nyumba ya Maaskofu, itapeleka nakala za muswada huo kwa Halmashauri za Dayosisi kupata maoni yao.

(3) Maoni toka Halmashauri za Dayosisi yatapokelewa na Kamati ya Katiba, na baada ya kuyafanyia kazi, mapendekezo yatarudishwa kwenye Nyumba ya Maaskofu. Baada ya kupata kibali cha Nyumba ya Maaskofu, Kamati itawasilisha muswada wa marekebisho ya Katiba kwenye Sinodi ya Kanisa kwa uamuzi.

(4) Marekebisho ya Katiba yatapitishwa kwa kura ya theluthi mbili ya kila Nyumba ya Sinodi.

## SURA YA KUMI NA TATU

## KANUNI ZA KANISA

### KANUNI YA KWANZA

**Uchaguzi wa Askofu Mkuu**

(1) Miezi mitatu kabla ya muda wa Askofu Mkuu aliyeko madarakani kumalizika au baada ya kiti cha Askofu Mkuu kuachwa wazi kwa sababu yoyote ile, Msajili wa Kanisa ataitisha Sinodi Maalum ya Uchaguzi.

(2) Uchaguzi wa Askofu Mkuu utafanyika hata kama kuna Dayosisi zisizozidi mbili ambazo hazina Maaskofu. Endapo kutakuwa na Dayosisi zaidi ya mbili hazina Askofu wa Dayosisi, basi uchaguzi wa Askofu Mkuu utaahirishwa mpaka zibakie sio zaidi ya Dayosisi mbili ambazo hazina Askofu wa Dayosisi.

(3) Uchaguzi wa Askofu Mkuu kama ukiahirishwa kama ilivyoelezwa kwenye ibara (2), basi Askofu Mkuu aliyeko ataendelea na wadhifa wake hadi uchaguzi utakapofanyika. Endapo nafasi ya Askofu Mkuu itakuwa wazi kutokana na sababu yoyote iliyotajwa katika Kifungu cha Nane cha Katiba hii, basi Makamu wa Askofu Mkuu ataendelea kukaimu.

(4) Wajumbe wote wa Sinodi Maalum ya Uchaguzi kabla hawajapiga kura wataahidi ifuatavyo: -

***"Nikifahamu umuhimu wa daraja takatifu la Askofu Mkuu, na jinsi ambavyo si haki itolewe isivyostahili, naahidi kwa dhati kwamba sitasema wala kupiga kura katika mkutano huu kwa woga au upendeleo, bali***

***kwa moyo mmoja kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kwa faida ya Kanisa lake, na kwa manufaa ya watu wake. Mungu unisaidie."***

(5) Katika kumchagua Askofu Mkuu utaratibu ufuatao utatumika:-

(a) Maaskofu wote wa Dayosisi wakiwemo Maaskofu wateule wa Dayosisi, isipokuwa wale waliotimiza miaka zaidi ya sitini (60), wana haki ya kupigiwa kura.

(b) Kura zitapigwa kwa siri, kila mjumbe akipiga kura moja.

(c) Kura zitapigwa kwa utaratibu wa kupunguza majina.

(d) Majina matatu tu yaliyopata kura nyingi katika kura ya kwanza yatachukuliwa na kupigiwa kura ya pili.

(e) Kura ya pili itapunguza jina moja kati ya matatu na kubakiza majina mawili.

(f) Kura ya tatu, mwenye jina lililopata kura nyingi atatangazwa kuwa Askofu Mkuu.

(g) Ikiwa kutakuwa na kura sawa katika kura ya tatu, uchaguzi utaahirishwa kwa muda na kuendelea siku hiyo hiyo. Endapo baada ya kura ya nne bado kuna kura sawa, Maaskofu watano wa Dayosisi waliowekwa wakfu awali ya wengine, ukiondoa wawili wanaopigiwa kura, watapiga kura. Askofu atakayepata kura nyingi atatangazwa kuwa Askofu Mkuu

(h) Iwapo katika upigaji kura wa awali, jina moja limepata kura zote, au robo tatu ya kura zote, Askofu huyo atatangazwa kuwa Askofu Mkuu.

(i) Uchaguzi ukiisha kufanyika, Nyumba ya Maaskofu watatia sahihi hati ya kuthibitisha na kutangaza jina la Askofu Mkuu aliyechaguliwa.

(j) Karatasi za kura zitatunzwa mahali pa siri kwa mwaka mmoja.

(k) Msajili wa Kanisa na Katibu Mkuu wa Kanisa watakuwa mashahidi watakaotia sahihi katika hati ya Maaskofu iliyotajwa katika ibara (ix) ndogo ya Kanuni hii.

**KANUNI YA PILI**

**Sifa za kuchaguliwa kuwa Askofu wa Dayosisi**

Sifa zinazotakiwa kwa uteuzi wa kuingia katika uchaguzi wa Askofu ni hizi zifuatazo:

(a) Umri kati ya miaka 40 – 60.
(b) Afya nzuri.
(c) Maisha na tabia yake iwe kama ielezwavyo hapa:
Sifa kama zilivyoainishwa katika 1Timotheo 3:1- 7 na Tito 1:7-9

i. Mbunifu.
ii Mtulivu.
iii Mtu wa watu
iv. Asiye na ubaguzi.
v Aliye tayari kujifunza na kupokea ushauri.
vi. Mpenda haki na amani.

(d) Awe kasisi mwenye uzoefu wa zaidi ya miaka mitano.

(e) Awe mwenye elimu ya kutosha:
   i. Awe na Diploma ya Theologia au kuzidi hapo; na
   ii. Awe na uwezo wa kuwasiliana kwa njia ya
   Kiswahili na Kiingereza.

(f) Mke wa Kasisi, kama anaye, awe:
   i. Anayeshuhudiwa mema katika jamii
   ii. Aliyekomaa kiroho; na
   iii. Mwenye msaada kwa huduma ya mume wake.

**KANUNI YA TATU**

**Wajumbe wa Sinodi**

Sinodi ya Kanisa itakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) Wajumbe kwa sababu ya vyeo vyao:
   (i) Askofu Mkuu;Makamu wa Askofu Mkuu;
   (ii) Maaskofu wa Dayosisi zote;
   (iii) Mhazini wa Kanisa;
   (iv) Msajili wa Kanisa;
   (v) Katibu Mkuu wa Kanisa;
   (vi) Mwenyekiti wa Kanisa wa UMAKI;
   (vii) Mwenyekiti wa TAYO; na
   (viii) Mama Mkuu wa CMM.

(b) Wajumbe wa kuchaguliwa na Sinodi za Dayosisi:
   (i) Wahudumu wawili kutoka kila Dayosisi; na
   (ii) Walei wawili kutoka kila Dayosisi (mmoja mwanaume na mmoja mwanamke).

## KANUNI YA NNE

**Msajili wa Kanisa**

(a) Kutakuwa na Msajili wa Kanisa ambaye atakuwa ni mwanasheria Mwanglikana na ambaye atachaguliwa na Sinodi ya Kanisa.

(b) Kila Dayosisi itakuwa na Msajili wake, ambaye lazima awe ni mwanasheria Mwanglikana, na kwa wadhifa huo ni Naibu Msajili wa Kanisa.

(c) Ikiwa Msajili wa Kanisa hawezi kuendelea kutimiza wajibu wake, Askofu Mkuu atafanya uteuzi maalum, akishauriana na Nyumba ya Maaskofu

(d) Wajibu wa Msajili wa Kanisa ni:

i. Kumshauri Askofu Mkuu katika mambo yote yanayohusu sheria.

ii. Kuhudhuria vikao vya Sinodi ya Kanisa, Halmashauri ya Kudumu na Nyumba ya Maaskofu (kama akihitajiwa).

iii. Kwa niaba ya Askofu Mkuu, kutekeleza mambo ya kisheria wakati wa kuamriwa Askofu au Askofu Mkuu, na wakati ambapo hati za sheria zinahitajika

iv. Madaraka mengine yoyote atakayopewa na Katiba hii au Sinodi ya Kanisa.

(e) Msajili wa Kanisa atachaguliwa kwa miaka mitatu na anaweza kuchaguliwa tena kwa miaka mingine mitatu mitatu.

## KANUNI YA TANO

**Kamati ya Fedha**

(a) Sinodi ya Kanisa itaunda Kamati ya Fedha itakayokuwa na uwezo kushughulikia mambo yote ya fedha ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

i. Mwenyekiti ambaye ni Askofu;

ii. Katibu Mkuu;

iii. Mhasibu wa Kanisa; na

iv. Wajumbe wengine wasiopungua wanne na wasiozidi sita wenye ujuzi wa mambo ya fedha na utumishi.

(b) Kazi za Kamati zitakuwa kama zifuatazo:-

i. Kutafuta na kupanga utumiaji wa fedha za Kanisa;

ii. Kutoa taarifa ya fedha na mali iliyokaguliwa kila mwaka kwa Halmashauri ya Kudumu;

iii. Kutoa taarifa ya fedha na mali kwa Sinodi ya Kanisa;

iv Kupanga mishahara na posho za watumishi wa Kanisa na idara zote;

v. Kupanga posho za wajumbe wa Kamati, Bodi, Jumuiya na wawakilishi mbalimbali za Kanisa.

vi. Kuandaa mapendekezo ya Kanuni za Utumishi na kuyawasilisha kwa Maofisa; na

vii. Kazi nyingine itakayopewa na Sinodi ya Kanisa au Halmashauri ya Kudumu au Nyumba ya Maaskofu.

**KANUNI YA SITA**

**Katibu Mkuu wa Kanisa**

(a) Kutakuwa na Katibu Mkuu wa Kanisa atakayeteuliwa na Nyumba ya Maaskofu.

(b) Katibu Mkuu ataajiriwa kwa mkataba wa miaka mitano na anaweza kuongezewa mikataba mingine isiyozidi miaka mitano mitano kama itakavyoonekana inafaa.

Isipokuwa kama Katibu Mkuu atakuwa hayupo au hawezi kutekeleza wajibu wake kwa sababu yoyote ile, Nyumba ya Maaskofu itateua Kaimu Katibu Mkuu au itafanya uamuzi mwingine wowote kadri itakavyoonekana inafaa.

(c) Kazi za Katibu Mkuu zitakuwa kama zifuatazo:-

i. Mtendaji Mkuu wa Kanisa;
ii. Msimamizi wa Idara, Jumuiya na Mashirika ya Kanisa;
iii. Katibu wa Nyumba ya Maaskofu;
iv. Kuandaa na kuwezesha vikao vya Sinodi, Halmashauri ya Kudumu na Kamati na Bodi zote za Kanisa;
v. Kutunza mahusiano mazuri na mashirika ya nje;
vi. Kutekeleza maazimio ya mikutano yote chini ya uongozi wa Askofu Mkuu;
vii. Kutunza kumbukumbu za mikutano na nyaraka za Kanisa;
viii. Kutunza Muhuri wa Wadhamini; na
ix. Kupokea mapendekezo ya agenda za Sinodi na Halmashauri ya Kanisa kutoka

Dayosisi na kuziwasilisha kwa Maafisa kabla ya kupelekwa kwa Nyumba ya Maaskofu.

x. Kazi nyingine zozote atakazopangiwa na Sinodi ya Kanisa au Halmashauri ya Kudumu au Nyumba ya Maaskofu.

**KANUNI YA SABA**

**Kuigawa Dayosisi**

(1) Endapo Askofu wa Dayosisi au Halmashauri ya Kudumu, wakiona haja ya kuigawa Dayosisi na kuifanya Dayosisi mpya au kumega sehemu na kufanya sehemu ya Dayosisi nyingine watashauriana baina yao wenyewe na kupeleka hoja kwenye Sinodi ya Dayosisi.

(2) Vigezo vya kuangaliwa katika kuigawa au kuimega Dayosisi ni vifuatavyo:
- (i) Kuwepo Wakristo wa kutosha;
- (ii) Uwezo wa kujiendesha kifedha;
- (iii) Kuwepo Majengo ya ofisi na nyumba za kuishi;
- (iv) Uwezekano wa kukua kwa Kanisa katika eneo hilo;
- (v) Kuwepo Wahudumu wa kutosha; na
- (vi) Kuwepo usafiri wenye uhakika kwa matumizi ya Dayosisi.
- (vii) Kuwepo mawasiliano kwa mfano simu na barabara.
- (viii) Makao makuu ya Dayosisi yawepo katika makao makuu ya Wilaya au Mkoa.

(3) Askofu wa Dayosisi inayohusika atapeleka kwa Askofu Mkuu:
- (i) Pendekezo la kutaka kuigawa na kuimega Dayosisi kufanya hivyo katika maandishi;
- (ii) Ushahidi wa kutimizwa vigezo vilivyotajwa kwenye kanuni ndogo (2) ya Kanuni hii;

(iii) Mipaka mipya inayopendekezwa; na
(iv) Eneo la Dayosisi litakalobaki chini ya mamlaka yake.

(4) Askofu Mkuu akipata taarifa zilizotajwa kwenye kanuni ndogo (3) ya Kanuni hii, atachuku hatua zifuatazo:

(i) Ataunda Tume ya Muda ambayo itaripoti kwake kuhusu kuwepo kwa vigezo vilivyotajwa;
(ii) Atashauriana na Nyumba ya Maaskofu baada ya kupata ripoti ya Tume ya Muda; na
(iii) Atapeleka suala hilo kwenye Halmashauri ya Kudumu ya Kanisa ili kutoa kibali kuanzishwa Dayosisi mpya au kumegwa Dayosisi moja na kipande kuunganishwa na Dayosisi nyingine.

(5) Baada ya Halmashauri ya Kudumu kutoa kibali, Dayosisi mama itapeleka kwenye Kamati ya Katiba ya Kanisa nakala ya Katiba mpya inayopendekezwa pamoja na nakala za Katiba ya Dayosisi mama ambayo imerekebishwa kama ipasavyo.

(6) Kamati ya Katiba ya Kanisa itatoa taarifa kwa Askofu Mkuu baada ya kuzipitia hizo Katiba na kuzifanyia marekebisho, kama itabidi.

(7) Askofu Mkuu atamuarifu Askofu wa Dayosisi inayohusika kwamba ombi la kugawa au kuimega Dayosisi limekubaliwa na ataagiza taratibu za uchaguzi wa Askofu chini ya Katiba hii zianze.

## KANUNI YA NANE

**Gharama za mikutano ya Kanisa**

(a) Dayosisi italipia gharama za usafiri wa kwenda na kurudi kwa wajumbe wa mikutano ya Sinodi ya Kanisa, na fedha za kujikimu (malazi na chakula) wakati wote wa mikutano.

(b) Ofisi Kuu ya Kanisa itagharimia:-

(i) Usafiri na fedha za kujikimu kwa wajumbe wa mikutano ya Sinodi Maalum ya Uchaguzi na Nyumba ya Maaskofu.

(ii) Usafiri na fedha za kujikimu kwa wajumbe wa Halmashauri ya Kudumu na Kamati na Bodi mbalimbali za Sinodi.

## KANUNI YA TISA

**Agenda za Sinodi ya Kanisa**

1. Utaratibu wa vikao vya kawaida vya Sinodi ni kama ifuatavyo:

(a) Katibu Mkuu wa Kanisa atatoa tangazo la kuitisha Mkutano wa Sinodi miezi tisa kabla ya mkutano.

(b) Mapendekezo ya agenda za Sinodi ya Kanisa yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Kanisa Anglikana Tanzania miezi sita kabla ya mkutano kutoka kwa:

(i) Sinodi za Dayosisi au Halmashauri za Kudumu za Dayosisi
(ii) Maaskofu wa Dayosisi
(iii) Kamati na Bodi za Kanisa
(iv) UMAKI
(v) TAYO; na
(vi) CMM

(c) Agenda zitawasilishwa na Katibu Mkuu wa Kanisa mwezi mmoja kabla ya kikao cha Sinodi kwa wale walioainishwa katika ibara

(d) Mwenyekiti wa Sinodi, kwa hiari yake, anaweza kuruhusu kuingiza agenda iliyochelewa kuwasilishwa.

2. Utaratibu wa Vikao Maalum vya Sinodi ni kama ifuatavyo:

(a) Katibu Mkuu wa Kanisa atatoa tangazo la kuitisha Kikao Maalum cha Sinodi, pamoja na agenda, miezi miwili kabla ya Kikao

## KANUNI YA KUMI

**Kamati ya Katiba**

(1) Kutakuwepo na Kamati ya Katiba ambayo itachaguliwa na Sinodi ya Kanisa ikiwa na wajumbe wafuatao:-

a) Mwenyekiti ambaye ni Askofu wa Dayosisi;
b) Katibu ambaye ni Katibu Mkuu wa Kanisa;
c) Msajili wa Kanisa;
d) Mjumbe mmoja kutoka Nyumba ya Maaskofu;
e) Wajumbe wawili kutoka Nyumba ya Wahudumu;
f) Wajumbe wawili kutoka Nyumba ya Walei (mwanamke mmoja na mwanamume mmoja).

(2) Kazi za Kamati ya Katiba zitakuwa kama ifuatavyo:

a) Kushughulikia mambo ya Katiba hii, na Katiba za Dayosisi.

(b) Kutoa mapendekezo yatakayosaidia na kuboresha uendeshaji wa Kanisa kikatiba

## KANUNI YA KUMI NA MOJA

**Bodi ya Mfuko wa Akiba**

(1) Kutakuwepo na Mfuko wa Pensheni wa Kanisa (Provincial Pension Fund), ambao utaitwa Mfuko katika Kanuni hii, ambao utachangiwa na wote waliomo katika Daraja Takatifu.

(2) Mfuko utaendeshwa na Bodi ya Mfuko wa Pensheni itakayoundwa na Sinodi ya Kanisa.

(3) Kila Dayosisi itawasilisha kwenye Mfuko michango ya walio katika Daraja Takatifu kila mwezi kwa viwango vilivyoidhinishwa na Bodi

(4) Kazi za Bodi ni:

a) Upokeaji wa michango ya akiba toka kila Dayosisi;

b) Kuwekeza (invest) michango hiyo ili kuongeza ukubwa wa mfuko;

c) Kutoa taarifa ya fedha kila mwaka kwa Halmashauri ya Kudumu;

d) Kutoa taarifa ya fedha kwa Sinodi ya Kanisa; na

e) Kuweka utaratibu na kusimamia ugawanyaji wa mafao kwa waliochangia Mfuko.

## KANUNI YA KUMI NA MBILI

**Bodi ya Elimu**

1. Kutakuwepo na Bodi ya Elimu ya Kanisa ambayo itaongoza na kusimamia Elimu katika Kanisa.

2. Bodi ya Elimu itakuwa na wajumbe wafuatao:

   (a) Mwenyekiti ambaye atakuwa Askofu wa Dayosisi.
   (b) Wakuu wa Vyuo vya Kanisa.
   (c) Wajumbe wengine wasiopungua wanne wenye taaluma ya elimu.

Kazi za Bodi ni:

a) Kuhakikisha kwamba Afisa Elimu wa Kanisa anatekeleza wajibu wake.

b) Kuajiri watumishi wa Idara ya Elimu ya Kanisa.

c) Kupitia na kuidhinisha mapendekezo ya maombi ya fedha kutoka Ofisi ya Afisa Elimu wa Kanisa.

d) Kupitia na kuidhinisha Bajeti ya Ofisi ya Elimu.

e) Kutafuta na kugawa rasilimali kwa kazi ya Elimu.

f) Kutekeleza maamuzi ya Sinodi na Halmashauri ya Kudumu yanayohusu Elimu.

g) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Kanisa Anglikana Tanzania.

h) Kuifanyia mapitio Sera ya Elimu ya Kanisa Anglikana Tanzania na kuomba idhini ya Halmashauri ya Kudumu na/au Sinodi ya Kanisa.

i) Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mbinu wa Elimu wa Kanisa.

**********************